UHAKIKA WA MAJI
Kwasababu sisi sote tupo mtoni

# Uhakika wa Maji kwa usawa na uendelevu wa Maji

Mradi wa Uhakika wa Maji, au kama ujulikanavyo kwa lugha ya Kiingereza *Fair Water Futures Programme* hufanya kazi na jamii, pamoja na serikali nchini Tanzania ili kuhakikisha kuwa rasilimali za maji katika mito, vijito au mikondo ya maji, maziwa na zile zilizopo chini ya ardhi zinasimamiwa kwa usawa na katika hali ya uendelevu – kwa manufaa ya wote. Mradi huu hutumia mbinu mpya za ubunifu ili kupelekea utekelezaji yakinifu wa sera za serikali, ikijumuisha ufuatiliaji wa uwajibikaji wa jamii, utetezi wenye ushahidi, na kujenga uwezo wa wataalamu wa sekta ya maji.

Shahidi wa Maji ni asasi ya kitanzania yenye makao yake mkoani Morogoro. Shirika linafanya kazi ya kipee kushawishi mabadiliko ya kisera nchini Tanzania ili kuleta usawa, ustadi na usimamizi endelevu wa rasilimali za maji. Kwa pamoja shirika la Shahidi wa Maji, *Water Witness International* na washirika wengine tunashirikiana katika utekelezaji wa mradi huu kwa ufadhili kutoka Taasisi ya Hewlett (*Hewlett Foundation*).

Lengo kuu ni kuzuia kupungua kwa wingi na ubora wa maji, migogoro, sawia na kujenga ustahimilivu wa tabia ya nchi kwa kukabiliana na mafuriko na ukame ili kuchagiza usawa na mustakabali wenye mafanikio kwa watanzania wote.



# Changamoto na Umuhimu wa Maji

Kukua kwa uchumi na kupungua kwa wimbi la umaskini kama itakavyo dira ya maendeleo ya Tanzania ya mwaka 2025, kunategemea kwa kiasi kikubwa utawala bora katika kuhakikisha rasilimali za maji zinatumiwa na kusimamiwa vizuri. Mradi wa Uhakika wa Maji unalenga kusaidia katika kuboresha sera na sheria mujarabu za Tanzania zinazohusu usambazaji na usimamizi wa rasilimali za maji ili kuwezesha maendeleo endelevu na ya usawa katika matumizi ya maji.

## Faida za Rasilimali za Maji kwa Tanzania: Maelezo kwa Ufupi[1]

### KILIMO

Kilimo kinatoa ajira kwa asilimia 50 ya watanzania na huchukua asilimia 89 ya matumizi ya maji. Changamoto kuu ni kupunguza kiasi cha maji yatumikayo katika kilimo na kwa wakati huohuo kuongeza uzalishaji wa chakula, ikiwa nchi inakusudia kuwa na maji ya kutosha kwaajili ya viwanda, uzalishaji wa nishati na usambazaji maji safi.

### NISHATI

Asilimia 42 ya umeme unaotumika nchini huzalishwa kwa maji. Shughuli za uzalishaji wa kiuchumi hutegemea sana umeme, ukusanyaji na uhifadhi mzuri wa maji ni muhimu kwa ongezeko la Pato la Taifa.

### USAMBAZAJI WA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA

Asilimia 63 ya idadi ya watu wanapata maji salama ya kunywa lakini ni asilimia 27 pekee wanaishi katika mazingira yenye huduma zilizoboreshwa za usafi wa mazingira, maji yana nafasi ya muhimu sana katika kuboresha afya na kuongeza nguvumali katika uzalishaji.

### WANYAMAPORI, MALIASILI NA UTALII

Misitu, uvuvi, mifugo na wanyamapori vyote ni tegemezi kwa maji kwa kiasi kikubwa, na vyote ni muhimu kwa uchumi na kujikimu. Utalii peke yake umeongeza asilimia 13 kwenye Pato la Taifa katika mwaka 2016. Usimamizi mbovu wa rasilimali za maji unaweza kuleta migogoro na hivyo kuhatarisha uhai wa viumbe hao.

### MABADILIKO YA HALI YA NCHI

Ukame na mafuriko vina madhara makubwa kiuchumi. Kiasi cha madhara haya inakadiriwa kuongezeka kwa kadri mabadiliko ya tabia nchi yanavyoendelea. Kutokana na matukio yasababishwayo na hali ya hewa na hasa ukame, inakadiriwa kuwa kila mwaka sekta ya kilimo hupoteza kiasi cha dola za kimarekani milioni 200 kwa wastani.

### VIWANDA

Ukuaji wa sekta za viwanda, madini na uzalishaji mali Tanzania unategemea kwa kiasi kikubwa rasilimali za maji. Usimamizi thabiti na utoaji maamuzi utahakikisha ukuaji wa sekta hizi hausababishi uchafuzi wa maji na matumizi yasiyo na kiasi kuathiri mazingira na watu.

Usimamizi mzuri wa maji ni muhimu katika kuboresha afya, namna za kujikimu (kuongeza ukwasi), fursa za kujiongezea kipato, na fursa za kiuchumi kwa jamii na watu walio kwenye mazingira hatarishi hasa watoto wa kike na wanawake.

Shahidi wa Maji inapigania mustakabali ambapo usimamizi wa rasilimali za maji utakua endelevu na

# Mbinu Zetu

Mradi wa Uhakika wa Maji unalenga kusaidia uhaishaji wa sera na sheria mujarabu za Tanzania ili kuwa na maendeleo endelevu na usawa katika matumizi ya maji. Mradi huu unafanya kazi na watumiaji wa maji, ukiwasaidia kuelewa haki na wajibu wao, na kuhaisha sera na sheria ili kupata haki za kisheria na ulinzi wa rasilimali za maji ambazo kimsingi, wanazihitaji kwa ukuaji wa uchumi na kuepuka umaskini. Mradi unafanikisha Uhakika wa Maji kupitia:

**Utafiti** – Tunafanya tafiti ili kubaini maeneo ambayo watumiaji wa maji hawajalindwa ipasavyo dhidi ya hatari kama uchafuzi na uhaba wa maji, uharibifu utokanao na mafuriko, ukame na migogoro.

**Uhamasishaji Jamii** – Tunafanya kazi na jamii ili kuwajengea uelewa wa haki na wajibu wao kama watumiaji wa maji, kuhaisha sera na sheria ili kutimiliza haki za kisheria na ulinzi wa rasilimali za maji ambazo kimsingi jamii inazihitaji kwa afya na ukuaji wa uchumi.

**Utetezi wenye Ushahidi** – Kufuatilia matokeo ya uhamasishaji wa jamii na kuchanganua ni jinsi gani rasilimali watu na fedha zinaweza kutumika katika kutoa ushahidi wenye mashiko kwa namna ambavyo utendaji kazi wa sekta unaweza kuboreshwa. Utetezi umelenga umma, watoa huduma, na wafanya maamuzi katika serikali na shughuli za kibiashara.

**Kusaidia Serikali na Shughuli za Kibiashara** – Kuchunguza jinsi gani taasisi zinatekeleza majukumu yake kikamilifu; kutoa ushauri wa kisera na kimchakato; na kujenga uwezo wa wataalamu kutokana na mahitaji. Pia, kusaidia makampuni ya Kibiashara kukidhi vigezo vya ubora wa kimataifa wa matumizi sahihi ya maji.

**Tathmini, Ufuatiliaji na Kujifunza** – Mradi wa Uhakika wa Maji unafuatilia kwa makini matokeo ya kazi zake ili kujifunza, kuboresha na kushirikisha mbinu na ushahidi wenye tija zaidi.

**‘Kuangazia nuru katika utendaji, na namna ambavyo pesa na rasilimali zinavyotumika haikuwahi kufanyika hapo awali. Kazi hii ni hatua kubwa kuelekea katika uwajibikaji mpana.’**

Bw. Nsaa-Iya Amaniel Kihunrwa, kutoka Sektretarieti ya Kikundi cha Wafadhili wa Miradi ya Maji, Tanzania

**‘Sekta ya maji inauhitaji muhimu sana wa sauti ya uwajijibikaji wa jamii na sauti hii ikichagizwa ndani ya asasi ya kiraia inakua ni bora na kamilifu zaidi.’**

Mhisani katika Sekta ya Maji

**‘Kwa mara ya kwanza watu wanadai haki zao juu ya maji. Hili ni ishara njema sana na itasaidia kuleta mabadiliko.’**

Bi. Praxeda Paul, Afisa Maji – Bonde la Wami/Ruvu



# Tunajivunia Nini Mpaka Leo?

Watu 224,601 wamenufaika kwa kuongezeka kwa uhakika wa maji. Kwa wastani, gharama za mradi zilizotumika ni sawa na shilingi 3000 tu kwa kila mnufaika.

Kwa kushirikiana na wabia wetu, pamoja na jamii tumeweza kung'amua changamoto na suluhisho la uchafuzi wa vyanzo vya maji unaotokana na shughuli za kibiashara na viwanda.

Uwasilishwaji wa Taarifa ya Mwaka Juu ya Hali ya Haki na Usawa katika Maji.

Tumeweza kuwa asasi ya kwanza ya kiafrika kuwa mwanachama wa Muungano wa Wasimamizi wa Maji (Alliance for Water Stewardship, AWS) na kuthibitishwa kwa cheti kama wakufunzi na washauri.

Uchambuzi wa Bajeti ya sekta ya maji na tathmini ya rasilimali ulitolewa.

Tuzo za Habari Za Maji: Ahadi ya Wizara kuhakikisha habari zinazohusu raslimali za maji zinasikika na kuandikwa kwa wingi.

Mbinu ya Kanuni za kutatua masuala hatarishi katika usimamizi wa rasilimali za maji ilikubaliwa na kuidhinishwa na Wizara na sasa inatekelezwa na Bodi za Maji za mabonde.

# Vipaumbele Vyetu kwa Wakati Ujao

## Tumeazimia kutekeleza yafuatayo katika mradi wetu wa Uhakika wa Maji:

- Kuainisha na kutanabaisha matokeo ya uwajibikaji wa jamii na kazi zetu za utetezi, sisi pamoja na washirika wetu ili kuchochea utekelezeji wa sheria za maji na kuleta Uhakika wa Maji kwa watu milioni moja wanaoishi katika mazingira hatarishi Tanzania;
- Kuweka wazi michango yetu yenye lengo la kuchochea mabadiliko ya kisera, kiutendaji na ufadhili wa miradi ya maji yenye mtazamo wa kusaidia watu wenye hali ngumu za kimaisha
- Kujengea uwezo unaolandana na mazingira ya pahali husika ili kuwasaidia washirika wetu kuwezesha Upatikanaji endelevu wa maji, kuunga mkono wananchi na asasi za kiraia katika kutia ari uwajibikaji wa jamii kwa wakati ujao.

# Ni Jinsi Gani Naweza Kushiriki?

Ili kufahamu zaidi juu ya Mradi huu, tutumie barua pepe kupitia anuani ifuatayo info@shahidiwamaji.org, au wasiliana na Meneja wa Mradi, Pendo Hyera kupitia anuani ya barua pepe, pendohyera@shahidiwamaji.org au tembelea tovuti yetu www.shahidiwamaji.org


## Anuani

Shahidi wa Maji,
Adrian Mkoba Memorial Building,
S.L.P 2527
Morogoro, Tanzania